MTANDAO WA MALEZI, MAKUZI NA MAENDELEO YA WATOTO WADOGO TANZANIA.

TANZANIA EARLY CHILDHOOD DEVELOPMENT NETWORK (TECDEN)

KATIBA YA MWAKA 2004

ILIYOYANYIWA

MAREKEBISHO MWAKA

2014

Yaliyomo

TAFSIRI YA MANENO iv
IBARA YA KWANZA – JINA, OFISI, LAKIRI NA NEMBO 1
1. Jina 1
2. Ofisi 1
3. Lakiri na Nembo 1
IBARA YA PILI - DIRA, DHIMA, MALENGO NA TUNU ZA MTANDAO 1
1. Dira 1
2. Dhima 1
3. Tunu za TECDEN 1
4. Lengo Kuu la Mtandao: 2
5. Malengo Mahususi: 2
IBARA YA TATU UANACHAMA, HAKI NA WAJIBU 2
1. Uanachama 2
a) Mwanachama wa Mtandao 2
b) Aina za Wanachama 2
c) Sifa za Mwanachama 3
d) Taratibu za kuomba Uanachama wa Mtandao 3
2. Haki na Wajibu wa Mwanachama 4
a) Haki ya Mwanachama 4
b) Wajibu wa Mwanachama 4
3. Kukoma na Kurejeshewa Uanachama 4
a) Kukoma Uanachama 4
b) Kurejeshewa Uanachama 5
IBARA YA NNE 5
MUUNDO WA UONGOZI NA USIMAMIZI WA MTANDAO 5
1. Mikutano ya Mtandao 5
a) Mkutano Mkuu 5
b) Mkutano Mkuu wa Dharura 6
c) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa 6
d) Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa 7
2. Muundo wa Bodi ya Mtandao 7
a) Wajumbe wa Bodi ya Mtandao 7
b) Sifa ya Wajumbe wa Bodi 8
c) Muda wa kuwa Mjumbe wa Bodi 8
d) Kukoma kuwa Mjumbe wa Bodi 8
e) Majukumu ya Bodi 9
f) Vikao vya Bodi ya Mtandao 9
g) Viongozi wakuu wa mtandao; 10
h) Kazi za Mwenyekiti wa Mtandao wa Taifa 10
i) Kazi za Makamu Mwenyekiti 10
3. Muundo na Kazi za Menejimenti 10
a) Muundo 10
b) Kazi za Menejimenti 10
c) Kazi za Mkurugenzi Mtendaji 10
4. Mikutano ya Mitandao ya Mikoa 11
a) Wajumbe wa Mkutano wa Mtandao ya Mkoa 11
b) Kazi za Mkutano wa Mtandao wa Mkoa 11

c) Kazi za Mwenyekiti wa Mtandao wa Mkoa 12
d) Kazi za Katibu wa Mtandao wa Mkoa 12
e) Kazi za Mratibu wa Mtandao wa Mkoa 12
f) Kazi za Mweka Hazina 13
IBARA YA TANO - UTUNZAJI WA FEDHA NA RASILIMALI ZA MTANDAO 13
1. Vyanzo vya Mapato ya Mtandao 13
2. Usimamizi wa Fedha na Raslimali 13
IBARA YA SITA – MAREKEBISHO/ABADILIKO YA KATIBA NA UTARATIBU WA KUYAFANYA MAREKEBISHO/MABADILIKO HAYO. 14
1. Marekebisho /Mabadiliko ya Katiba 14
2. Utaratibu wa kurekebisha Katiba 14
IBARA SABA - KUVUNJIKA KWA MTANDAO 14
IBARA YA NANE - KUANZA KUTUMIKA KWA KATIBA HII 15
IBARA YA TISA - UWAJIBIKAJI 15
IBARA YA KUMI - KUTHIBITISHA KATIBA 15

TAFSIRI YA MANENO

Katika katiba hii, isipokuwa itakapoelezwa vingenevyo, maneno yafuatayo yatatafsiriwa kama ifuatavyo:

Neno	Tafsiri
Akaunti ya Benki	Akaunti ya kuhifadhi fedha za Mtandao kama inavyoelekezwa katika Katiba hii.
Bodi	Chombo cha maamuzi kilichoundwa ili kufanya maamuzi kuelekeza, kushauri na kusimamia mwenendo na maendeleo ya Mtandao
Katibu	Kiongozi aliyechaguliwa kuratibu shughuli za wanachama wa Mtandao kwa mujibu wa kanuni za Katiba hii.
Maendeleo ya Mtoto	Hatua za mabadiliko ya mtoto yanayotokea hatua moja baada ya nyingine kulingana na umri wa mtoto, na ambayo yanamwezesha kushiriki kikamilifu katika maisha kulingana na hatua mbali mbali za makuzi yake
Mkaguzi wa Nje	Mtu/taasisi iliyopewa dhamana ya kukagua mwenendo na matumizi ya rasilimali za Mtandao kwa mujibu wa Katiba hii.
Menejimenti	Ni chombo cha kuratibu shughuli za kila siku za Mtandao kinachoundwa na watumishi walioajiriwa na Mtandao
Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao:	Ni kiongozi wa Menejimenti ya Mtandao na Katibu wa vikao vya Bodi na Mkutano Mkuu wa Mtandao.
Mtandao	Muungano wa vikundi , taasisi na mashirika yanayojishughulisha na masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ikiwemo utetezi wa haki na maslahi ya mtoto na shughuli zingine ambazo kwa namna moja au nyingine zinachangia kuboresha huduma jumuishi za Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM)
Mtoto	Mwanadamu kuanzia mimba hadi umri wa miaka nane
Mwaka wa Fedha	Kipindi cha miezi kumi na miwili ya utekelezaji wa mpango

	na bajeti ya Mtandao inayoanzia tarehe moja Januari na kuishia terehe thelathini na moja Disemba ya kila mwaka
Mwanachama	Kikundi, shirika; au taasisi iliyojiunga na Mtandao na iliyolipa kiingilio, ada na michango yote kwa mujibu wa kanuni za Katiba hii
Mwenyekiti	Kiongozi aliyechaguliwa na wanachama wa Mtandao kuongoza Mtandao/Bodi kwa mujibu wa Katiba hii
Wajumbe wa Bodi:	Watu waliochaguliwa na kuteuliwa kuunda Bodi ya Mtandao.

IBARA YA KWANZA – JINA, OFISI, LAKIRI NA NEMBO

1. Jina

Mtandao huu utajulikana kwa jina la Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania *(Tanzania Early Childhood Development Network-TECDEN)*

2. Ofisi

Mtandao utakuwa na ofisi za uratibu jijini Dar es Salaam na utafanya kazi na ofisi za mitandao ya mikoa, Tanzania Bara na Zanzibar.

3. Lakiri na Nembo

Mtandao utakuwa na lakiri itakayokuwa na jina la "**Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto Wadogo Tanzania**" likiwa limeandikwa kwa herufi kubwa na itakuwa na nembo inayoutambulisha Mtandao.

Lakiri hiyo itakuwa na umbile la duara na itapigwa kwenye nyaraka zote za kisheria mbele ya Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao au makamu wake na mjumbe mmoja wa Bodi.

IBARA YA PILI - DIRA, DHIMA, MALENGO NA TUNU ZA MTANDAO

1. Dira

Dira ya mtandao ni kuwa na Tanzania yenye watoto wanaopatiwa huduma bora za makuzi, malezi na maendeleo kwa ujumla wake

2. Dhima

Mtandao umedhamiria kufikia dira yake kwa kuhakikisha kuwa wanachama wote wa Mtandao wanafanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine ili kuendeleza mkabala wa kuunganisha sekta zote husika ambazo zinatilia mkazo maendeleo jumui ya mtoto na ambazo zinaakisi haki na sauti za watoto wadogo katika masuala yanayowahusu.

3. Tunu za TECDEN

a. Kuheshimu haki ya kila mtoto bila ubaguzi wa aina yoyote
b. Kumlinda mtoto dhidi ya unyanyasaji na ukatili wa aina yoyote.
c. Kusimamia ukweli na uwazi katika shughuli za Mtandao
   Uadilifu
d. Kufanya kazi pamoja na kwa kushirikiana.

4. Lengo Kuu la Mtandao:

Lengo kuu la Mtandao ni kujenga mazingira yatakayowezesha wanachama wa Mtandao na wadau wanaosaidia watoto wadogo katika ngazi zote za jamii na kitaifa kushiriki kikamilifu katika kuelimisha, kuhamasisha, kusimamia na kutetea haki na upatikanaji wa huduma jumuishi za Malezi, Makuzi na Mendeleao ya Awali ya Mtoto (MMMAM) kwa maisha na maendeleo ya watoto wadogo nchini.

5. Malengo Mahususi:

Malengo mahususi ya Mtandao ni pamoja na:

a. Kufanya ushawishi na utetezi wa masuala yanayohusu uboreshaji wa huduma na kulinda haki za watoto
b. Kuhamasisha jamii na watoa huduma kutambua umuhimu wa kuimarisha na kuwezesha watoto wadogo kupata mahitaji na haki zao za msingi.
c. Kushawishi maboresho ya sera na kufuatilia utekelezaji wa sheria na miongozo ya kuboresha huduma za watoto wadogo.
d. Kubuni na kuimarisha mifumo ya upashanaji habari na kuelimishana katika ngazi zote za huduma kwa watoto wadogo.
e. Kutafiti na kutumia matokeo ya utafiti katika kuboresha huduma kwa watoto wadogo.
f. Kujenga uwezo wa taasisi ya TECDEN na wanachama wake ili waweze kutoa huduma stahiki na endelevu kwa watoto wadogo nchini.

IBARA YA TATU UANACHAMA, HAKI NA WAJIBU

1. Uanachama

a) Mwanachama wa Mtandao

Mwanachama wa Mtandao ni kikundi, shirika au taasisi yoyote iliyoomba kwa hiari yake, na kukubaliwa kujiunga kama mmoja wa wadau wa Mtandao kwa mujibu wa masharti yaliyo katika ibara ndogo ya 1 – 4 ya ibara ya tatu

b) Aina za Wanachama

(i) Uanachama wa Mtandao utakuwa wa vikundi, shirika, jumuiya na taasisi

(ii) Taasisi/shirika litakalopewa heshima na kutambuliwa na Mkutano Mkuu

c) Sifa za Mwanachama

Mwombaji atakubalika kuwa mwanachama iwapo:

(i) Malengo au moja ya malengo ya kikundi , shirika jumuia au taasisi,inahusu masuala ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM) au shughuli zake zinachangia kuboresha huduma jumuishi za MMMAM

(ii) Anakubali kufuata masharti na kanuni kama ilivyoainishwa katika Katiba hii

(iii) Uwepo wake unatambulika kwa mujibu wa sheria za uanzishwaji wa vikundi shirika au taasisi husika.

(iv) Anakubalika na jamii anayoihudumia au anayofanyia kazi

(v) Hajishughulishi na masuala ya kisiasa kwa namna moja au nyingine

d) Taratibu za kuomba Uanachama wa Mtandao

(i) Mwombaji mpya wa uanachama wa Mtandao atatuma maombi kwa Katibu/mratibu wa mtandao wa TECDEN wa mkoa husika.

(ii) Mwombaji ataonesha mashahidi wasiopungua wawili (2) wanaofahamika na Mtandao , ambao wanaweza kuulizwa kuhusu taarifa, mwenendo na tabia ya mwombaji inapolazimika. *Kwa maombi yote, mdhamini anaweza kuwa taasisi ya jamii au ya umma, jumuia, kikundi au shirika lingine linalofahamika.*

(iii) Mwombaji anaweza kutakiwa kutoa maelezo ya ziada ya kuwezesha ofisi ya Mtandao kufanya maamuzi.

(iv) Katibu/Mratibu wa Mtandao ngazi ya Mkoa atapitia na kuwakilisha maombi mapya ya wanachama katika kila kikao cha uongozi wa Mkoa kwa maamuzi ya kuyapokea au kuyakataa

(v) Mwombaji atafahamishwa matokeo ya maombi yake mara baada ya kikao husika na kutakiwa kujaza fomu maalumu ya uanachama .

(vi) Mwombaji wa uanachama aliyekubaliwa atatakiwa kulipa kiingilio na ada ya kila mwaka na kwa viwango kama itakavyoelekezwa mara kwa mara na Bodi ya mtandao kulingana na masharti ya katiba hii.

(vii) Wanachama wa heshima watatambuliwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mtandao na watathibitishwa na Mkutano Mkuu wa Mtandao wa kitaifa.

2. Haki na Wajibu wa Mwanachama

a) Haki ya Mwanachama

Kila mwanachama wa Mtandao ana haki zifuatazo:

(i) Kushiriki katika shughuli zote za kuimarisha Mtandao na Maendeleo ya watoto wadogo Tanzania

(ii) Kushiriki katika vikao na mikutano yote itakayoandaliwa na Mtandao katika ngazi husika

(iii) Kupatiwa au kutaarifiwa habari zozote zinazohusu maendeleo ya watoto na taasisi kwa ujumla.

(iv) Kupiga/Kupigiwa kura na kuchaguliwa katika nafasi zozote za uongozi wa Mtandao.

(iii) Kukata rufaa kwenye ngazi ya juu endapo ataona hakuridhishwa na maamuzi yaliyochukuliwa na ngazi husika yanayohusu uanachama wake.

b) Wajibu wa Mwanachama

Kila mwanachama wa Mtandao atakuwa na wajibu wa kuuwezesha Mtandao kutimiza madhumuni yake kama ifuatavyo:

(i) Kuheshimu na kulinda Katiba ya Mtandao

(ii) Kulipa kiingilio na ada ya kila mwaka na michango mingine yoyote itakayoamuliwa na Mtandao

(iii) Kutekeleza kwa ukamilifu kanuni na/au miongozo mbali mbali ya mtandao

(iv) Kutoa taarifa zote muhimu kwa faida ya wanachama na wadau wengine

(v) Kutekeleza shughuli za MMMAM na kutoa taarifa kwenye ngazi husika ya Mtandao

3. Kukoma na Kurejeshewa Uanachama

a) Kukoma Uanachama

Mwanachama anaweza kukoma kuwa mwanachama wa Mtandao endapo;

(i) Atajitoa kwa hiari yake mwenyewe kwa taarifa ya maandishi

(ii) Atashindwa kutimiza masharti na wajibu wake wa Kikatiba kama ilivyoainishwa katika ibara ya 3.2 (wajibu na majukumu) na kama itakavyofafanuliwa katika Katiba hii

(iii) Kuondolewa na maamuzi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutokana na sababu zitakazoakisi uamuzi huo kufikiwa

(iv) Taasisi kufungwa

(v) Taasisi ikibadilisha malengo yake

b) Kurejeshewa Uanachama

Mwanachama yeyote ambaye uanachama wake ulisitishwa au kukoma kwa mujibu wa vifungu vilivyo chini ya ibara ndogo ya 3.3.1 hapo juu, anaweza kuomba kurejeshewa uanachama wake;

(i) Kwa kuomba upya kwa maandishi akithibitisha kuwa ameweza kurekebisha makosa yaliyosababisha afukuzwe. Maombi yake yatajadiliwa na ya Bodi ya Mtandao

(ii) Endapo atakubaliwa kurejeshewa uanachama, atakubaliana na masharti yote yatakayotolewa na Mkutano Mkuu

IBARA YA NNE

MUUNDO WA UONGOZI NA USIMAMIZI WA MTANDAO

Mtandao utakuwa na muundo wa uongozi wenye ngazi zifuatazo;

1. Mkutano Mkuu wa Taifa
2. Bodi ya Mtandao
3. Mkutano Mkuu wa Mkoa
4. Menejimenti ngazi ya Taifa
5. Menejimenti ngazi ya Mkoa

1. Mikutano ya Mtandao

a) Mkutano Mkuu

(i) Mkutano Mkuu wa Taifa ndicho chombo chenye mamlaka ya juu kabisa kwenye Mtandao na chenye maamuzi ya mwisho kuhusiana na shughuli na mwenendo wa Mtandao.

(ii) Mkutano Mkuu wa Mtandao utafanyika mara moja kila baada ya Mwaka kwa tarehe, muda na mahali patakapopendekezwa na menejimenti ya Mtandao wa Taifa.

Taarifa ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu itatolewa na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kwa njia ya maandishi angalau siku ishirini na moja (21) kabla ya tarehe ya mkutano. Taarifa hii itarudiwa tena angalau siku Saba (7) kabla ya siku ya Mkutano.

(iii) Akidi ya Mkutano Mkuu ni theluthi mbili ya wajumbe wote halali na wenye haki ya kupiga kura

(iv) Hakuna shughuli yoyote inayohusu Mkutano Mkuu itaruhusiwa kufanyika hadi Akidi imekamilika katika muda uliopangwa kuanza kwa mkutano huo

(v) Kila mwanachama halali atakuwa na kura moja tu. Endapo kura zimelingana upigaji kura utarudiwa, endapo kura zitalingana tena, Mwenyekiti atapiga kura ya uamuzi.

(vi) Upigaji wa kura katika Mkutano Mkuu utakuwa wa siri na uamuzi utafikiwa kwa wingi wa kura

b) Mkutano Mkuu wa Dharura

(i) Mwenyekiti, anaweza kuitisha Mkutano wa dharura kutokana na maombi ya maandishi kutoka kwa angalau theluthi moja ya wajumbe halali wa Mkutano Mkuu.

(ii) Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao atatoa notisi ya taarifa angalau siku saba (7) kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu wa Dharura kufanyika

(iii) Mkutano wa Dharura utaendeshwa kwa taratibu kama zile za Mkutano mkuu kwa kuzingatia agenda za mkutano wa dharura

c) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Mtandao utakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Wajumbe wote wa Bodi ya Mtandao

(ii) Wawakilishi wawili watakao chaguliwa na Mkutano Mkuu wa mkoa kutoka kwenye mitandao hai ya mikoa

(iii) Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao akiwa katibu na mjumbe asiye piga kura

(iv) Wageni waalikwa kutoka miongoni mwa wadau , kadiri Bodi itakavyoona inafaa na ambao hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

d) Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na kazi kuu zifuatazo:

(i) Kumchagua Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu husika.

(ii) Wakati wa mkutano mkuu wa uchaguzi, Kumchagua mwenyekiti na wajumbe wa Bodi ya mtandao

(iii) Wakati wa Mkutano Mkuu wa uchaguzi, kuthibitisha uteuzi wa wajumbe wa Bodi watakaotokana na wanachama wa heshima.

(iv) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa za mwaka za utekelezaji wa mipango na ukaguzi wa matumizi ya fedha za Mtandao.

(v) Kupokea na kuthibitisha mpango kazi wa mwaka.

(vi) Kuchagua na kuwajibisha Bodi ya Mtandao

(vii) Kuthibitisha Mkaguzi wa nje wa mahesabu ya Mtandao.

(viii) Kupanga viwango vipya vya kiingilio na michango mingine ya wanachama wa Mtandao.

(ix) Kufanya marekebisho ya Katiba hii kama itakavyohitajika na wanachama au mamlaka za kisheria.

(x) Kupitisha sera na kuidhinisha kanuni na miongozo ya mtandao

2. Muundo wa Bodi ya Mtandao

a) Wajumbe wa Bodi ya Mtandao

Kwa kuzingatia sifa na vigezo vya wajumbe wa bodi kama itakavyofafanuliwa kwenye kanuni na miongozo, Bodi ya Mtandao itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Wajumbe watano (5) akiwemo Mwenyekiti na makamu wake watakao chaguliwa miongoni mwa wanachama hai wa Mtandao.

(ii) Wajumbe wawili (2) kutoka nje ya wanachama wa Mtandao kama watakavyopendekezwa na Bodi na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa Mtandao

(iii) Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao.

b) Sifa ya Wajumbe wa Bodi

Mjumbe wa Bodi anatakiwa kuwa na sifa sifuatazo;

(i) Mwenye uzoefu katika uongozi na utashi wa kufanya kazi za Malezi Makuzi na Maendeleo ya watoto wadogo.

(ii) Anayeonesha utayari wa kujituma na kujitolea kusaidia utekelezaji wa kazi za Mtandao

(iii) Mwenye ari ya kujifunza na kubadilishana uzoefu na wengine

(iv) Awe na elimu kiwango cha Diploma au zaidi

(v) Awe amekidhi vigezo vitakavyowekwa kwenye kanuni za uchaguzi

c) Muda wa kuwa Mjumbe wa Bodi

(i) Wajumbe wa Bodi watadumu katika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu (3), na baada ya hapo wajumbe wapya watachaguliwa.

(ii) Wajumbe wa Bodi wanaomaliza muda wao wanaweza kuchaguliwa tena kuendelea nafasi zao kwa kipindi kingine cha miaka mitatu endapo watachaguliwa.

(iii) Hata hivyo, kila wakati wa uchaguzi, theluthi moja ya wajumbe wanaomaliza muda wao wa miaka mitatu (3) watatakiwa waachie nafasi kwa wajumbe wapya. Bodi itakuwa na theluthi mbili ya wajumbe wanaoendelea ili kuendeleza kumbukumbu ya kitaasisi.

(iv) Ukomo wa mjumbe kutumikia uongozi ni awamu mbili tu

d) Kukoma kuwa Mjumbe wa Bodi.

Mjumbe wa Bodi anaweza kukoma kuwa mjumbe kutokana na moja ya sababu zifuatazo:

(i) Endapo Mjumbe ataomba kuacha kwa hiari yake mwenyewe

(ii) Endapo wanachama hawataridhika na utendaji wake wa kazi na kupigiwa kura ya kutokuwa na imani kupitia Mkutano Mkuu

(iii) Endapo mjumbe hatapigiwa kura na wajumbe wa Mkutano Mkuu katika uchaguzi

(iv) Endapo Mjumbe wa Bodi ameonekana kutotimiza matarajio ya Mtandao na masharti ya Katiba hii

(v) Endapo Mjumbe amefariki.

(vi) Endapo Mtandao utavunjika au kuvunjwa kisheria.

(vii) Endapo Mjumbe atahukumiwa na kufungwa kutokana na makosa ya jinai.

(viii) Endapo Mjumbe hatahudhuria vikao vya Bodi kwa vipindi vitatu mfululizo bila taarifa kwa Mwenyekiti

e) Majukumu ya Bodi

(i) Kutunga sera, kanuni na miongozo ya Mtandao

(ii) Kupitisha mpango mkakati na mpango kazi wa Mtandao

(iii) Kuthibitisha taarifa ya utekelezaji na taarifa ya ukaguzi

(iv) Kuajiri au kusitisha ajira za watendaji wa Mtandao .

(v) Kuimarisha mahusiano baina ya wanachama na wadau wengine kwa lengo la kutangaza Mtandao kwa upana wake

(vi) Kupendekeza majina ya wakaguzi wa nje wa hesabu za Mtandao na kuwasilisha kwa Mkutano Mkuu kwa idhini.

(vii) Kupendekeza majina ya wajumbe wapya wa Bodi ambao ni wanachama wa heshima na kuwasilisha kwa Mkutano Mkuu wa Mtandao kwa uthibitisho.

(viii) Kutafuta rasilimali na au kupendekeza njia mbadala na endelevu za vyanzo vya fedha na raslimali zingine kwa ajili ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Mtandao

(ix) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Mtandao.

(x) Kumchagua Makamu mwenyekiti wa Bodi kwenye kikao chake cha kwanza baada ya uchaguzi.

(xi) Kuunda kamati ndogo ndogo kulingana na mahitaji kama zitakavyofafanuliwa katika Kanuni za Mtandao.

f) Vikao vya Bodi ya Mtandao

(i) Vikao vya Bodi vitafanyika mara nne kwa mwaka

(ii) Mkurugenzi Mtendaji kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Bodi watapendekeza tarehe, mahali na muda wa Mkutano na kuwafahamisha wajumbe wote kwa notisi ya maandishi au njia yoyote ya mawasiliano muafaka, angalau siku kumi na nne (14) kabla ya tarehe ya mkutano.

(iii) Akidi ya Mkutano wa Bodi ni theluthi mbili ya wajumbe wote halali na wenye haki ya kupiga kura

g) Viongozi wakuu wa mtandao;

Viongozi wakuu wa mtandao watakuwa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji. .

h) Kazi za Mwenyekiti wa Mtandao wa Taifa

(i) Kuendesha vikao vya Bodi ya Mtandao

(ii) Kuwakilisha Mtandao katika mialiko ya mikutano na mijumuiko mingine ndani na nje ya nchi inayohusu maswala ya Mtandao.

(iii) Mwenyekiti ndiye msemaji mkuu wa Mtandao

(iv) Kuitisha vikao vya Mtandao kitaifa

(v) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yote ya Bodi na Mkutano Mkuu

i) Kazi za Makamu Mwenyekiti

Endapo Mwenyekiti hatakuwepo, kazi zake zitafanywa na makamu mwenyekiti

3. Muundo na Kazi za Menejimenti

a) Muundo

Menejimenti ya Mtandao itaundwa na watumishi walioajiriwa na mtandao

b) Kazi za Menejimenti

(i) Kuratibu na Kutekeleza shughuli za kila siku za mtandao

(ii) Kubuni miradi na Kutafuta rasilimali za kutekeleza shughuli za Mtandao

(iii) Kutunza kumbukumbu za wanachama wa Mtandao

(iv) Kupokea maombi /orodha ya wanachama wapya kutoka kwa waratibu /makatibu wa Mitandao ya Mikoa

(v) Kuandaa na kuratibu mikutano, makongamano na majukwaa mbalimbali ya kuwezesha wanachama na wadau wengine kujadili masuala ya watoto wadogo.

(vi) Kuandaa vikao vya Bodi

(vii) Kuandaa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa shughuli za Mtandao

c) Kazi za Mkurugenzi Mtendaji

Mkurugenzi Mtendaji wa mtandao ndiye msimamizi na mtendaji Mkuu wa shughuli za kila siku za Mtandao

(i) Ndio kiongozi mkuu wa menejimenti ya Mtandao Kitaifa

(ii) Kusimamia uratibu na kuunganisha shughuli za wanachama na wadau wengine wa Mtandao

(iii) Kuratibu mikakati na mipango ya utekelezaji wa shughuli za Mtandao

(iv) Kuwa Afisa mthibiti wa fedha na raslimali za Mtandao wa Mtandao

(v) Kutoa taarifa za matumizi na ukaguzi wa fedha na raslimali za Mtandao kwenye vikao vya Bodi

(vi) Atawakilisha Mtandao katika vikao na mihadhara yote halali ya kitaalamu na kiutendaji ndani na nje ya Nchi

(vii) Kutafuta raslimali za kutekeleza mipango ya mtandao

(viii) Kufanya shughuli zingine za mtandao atakazoagizwa na Bodi

4. Mikutano ya Mitandao ya Mikoa

Kutakuwa na Mikutano ya Mitandao ya Mkoa itakayofanyika mara moja kila mwaka kabla ya Mkutano Mkuu wa Taifa

a) Wajumbe wa Mkutano wa Mtandao ya Mkoa

Mkutano Mkuu wa Mtandao wa Mkoa utajumuisha wajumbe wafuatao:

(i) Wawakilishi wawili (2) kutoka kila taasisi/shirika mwanachama wa mtandao kwa kuzingatia jinsia.

(ii) Mjumbe wa Bodi ya Mtandao Taifa aliyeko katika mkoa huo.

(iii) Viongozi wa Mkoa watatu (3) ambao ni Mwenyekiti, Katibu na Mweka hazina watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mkoa kwa mzunguko. Kwa mkoa wenye uwezo wataajiri mratibu ambaye naye atakuwa mjumbe asiye na uwezo wa kupinga kura

(iv) Wageni waalikwa.

b) Kazi za Mkutano wa Mtandao wa Mkoa

Mkutano wa Mkoa utakuwa na kazi zifuatazo:

(i) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa za mwaka za utekelezaji wa mipango, na ukaguzi wa matumizi ya fedha za mtandao.

(ii) Kuchagua viongozi wa Mtandao wa mkoa.

(iii) Kupokea na kuthibitisha mpango kazi wa mwaka unaofuata.

(iv) Kupokea na kupitisha maombi ya wanachama wapya na kutuma kumbukumbu makao makuu ya Mtandao wa Taifa

(v) Kusitisha uanachama wa wanachama wa Mtandao na kusuburi uthibitisho Mkutano Mkuu wa Taifa..

(vi) Kuchagua wajumbe wawili wa kuwakilisha mkoa katika Mkutano Mkuu wa Taifa.

c) Kazi za Mwenyekiti wa Mtandao wa Mkoa

(i) Kuendesha Mikutano yote ya Mtandao.

(ii) Kuwakilisha Mtandao katika mialiko ya mikutano na mijumuiko mingine ndani na nje ya mkoa

(iii) Mwenyekiti ndiye msemaji mkuu wa Mtandao endapo mwenyekiti hatakuwepo kazi zake zitafanywa na Katibu wa Mkoa.

(iv) Kuitisha vikao vya Mtandao kimkoa

d) Kazi za Katibu wa Mtandao wa Mkoa

(i) Kuwa Katibu wa vikao vyote vya mikutano ya uongozi wa Mkoa

(ii) Atafanya kazi zote za Mratibu wa Mkoa kwa mikoa ambayo haina uwezo wa kuajiri Mratibu.

e) Kazi za Mratibu wa Mtandao wa Mkoa

(i) Mratibu wa Mtandao ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za kila siku za Mtandao ngazi ya Mkoa

(ii) Kuratibu na kuunganisha harakati za wanachama na wadau wengine wa Mtandao katika Mkoa husika

(iii) Kutunza kumbukumbu za wanachama wa Mtandao nagazi ya Mkoa .

(iv) Kuandaa mikakati na mipango ya utekelezaji wa shughuli za Mtandao nagazi ya Mkoa

(v) Kuandaa taarifa za matumizi na ukaguzi wa fedha na raslimali za Mtandao

(vi) Kuandaa mikutano, makongamano na majukwaa mbalimbali ya kuwezesha wanachama na wadau kujadili masuala ya watoto wadogo.

(vii) Kupokea maombi ya wanachama wapya kwa mujibu wa katiba na kuyawasilisha kwa uongozi wa mkoa na Taifa

(viii) Kutafuta na kusimamia rasilimali za mtandao ngazi ya Mkoa

f) Kazi za Mweka Hazina

Atasimamia na kutunza kumbukumbu za fedha za mtandao ngazi ya Mkoa

IBARA YA TANO - UTUNZAJI WA FEDHA NA RASILIMALI ZA MTANDAO

1. Vyanzo vya Mapato ya Mtandao

Vyanzo vikuu vya upatikanaji wa fedha na rasilimali za Mtandao vitakuwa:

a) Kiingilio na michango ya mwaka ya wanachama wa mtandao kama itakavyopitishwa na Mkutano Mkuu

b) Michango ya hiari kutoka kwa marafiki na mitandao mingine

c) Misaada na ufadhili kutoka kwa wahisani wa ndani na nje ya nchi

d) Mauzo yanayotokana na vifaa chakavu vya Mtandao na nyenzo za ushawishi kama vile machapisho, fulana, kofia kalamu nk

e) Vyanzo vingine vyovyote ilimradi ni halali kisheria

2. Usimamizi wa Fedha na Raslimali

a) Fedha yote ya Mtandao itahifadhiwa katika akaunti yenye jina la Mtandao katika benki zinazotambulika kihalali.

b) Mtandao utaandaa na kufuata sera na mifumo ya usimamizi wa fedha kwa kiwango cha Kimataifa, zitakazoidhinishwa na Bodi.

c) Bodi itatafuta, itapitia na kupendekeza majina ya makampuni yenye sifa na uweledi yatakayofanya ukaguzi wa hesabu za Mtandao mwisho wa mwaka na kuyapeleka kwa Mkutano Mkuu kwa idhini.na.

d) Mkaguzi wa nje atafanya ukaguzi na kuthibitisha uhalali wa matumizi ya Mtandao na kutoa taarifa yake kwa Bodi.

e) Watia sahihi wa Mtandao ni kama itakavyoainishwa kwenye kanuni za fedha ya Mtandao

f) Mwaka wa fedha wa mtandao ni kuanzia tarehe moja Januari hadi tarehe thelathini na moja Disemba ya kila mwaka

IBARA YA SITA – MAREKEBISHO/ABADILIKO YA KATIBA NA UTARATIBU WA KUYAFANYA MAREKEBISHO/MABADILIKO HAYO.

1. Marekebisho /Mabadiliko ya Katiba

a) Katiba hii inaweza kufanyiwa marekebisho/mabadiliko kwa maombi ya theluthi mbili ya wajumbe wa Mkutano Mkuu, Mkutano wa kawaida au Mkutano wa Dharura ulioitishwa kwa madhumuni hayo.

b) Inaweza pia kufanyiwa marekebisho/mabadiliko kutokana na mahitaji ya wakati uliopo yaliyotokana na utafiti au mahitaji mengine ya dharura kuzingatia kipengele (i).

c) Katiba hii inaweza pia kufanyiwa marekebisho/mabadiliko kutokana na agizo la mamlaka zingine za serikali na za kisheria

2. Utaratibu wa kurekebisha Katiba

a) Notisi ya kutaka marekebisho ya Katiba itawasilishwa kwa Mwenyekiti, ambaye pia atatoa notisi kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu, akionesha aina ya mabadiliko yanayopendekezwa (kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kwa maandishi), angalau siku kumi na nne (14) kabla ya tarehe ambayo agenda inatakiwa kujadiliwa

b) Bodi inao uwezo wa kupendekeza marekebisho/ ya Katibakanuni, miongozo ili mradi mabadiliko hayo yata pelekwa na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu kabla ya kutumika.

c) Mabadiliko yatakayotokana na mahitaji ya wakati au utafiti yatajadiliwa kwenye Bodi na maeneo yenye kasoro kuwasilishwa kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kuidhinishwa

IBARA SABA - KUVUNJIKA KWA MTANDAO

a) Mtandao unaweza kuvunjika kwa makubaliano ya Mkutano Mkuu, Mkutano wa Kawaida na Mkutano wa Dharura ulioitishwa kwa madhumuni hayo.

b) Maamuzi ya kuuvunja Mtandao yatafikiwa na angalau theluthi mbili ya wajumbe halali wa Mkutano Mkuu husika

c) Pendekeo la uamuzi wa kuvunja Mtandao litawasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao angalau siku ishirini na moja (21) kabla ya kikao kilichopendekezwa kujadili suala hilo.

d) Pendekezo la uamuzi wa kuvunja Mtandao litajumuisha na mapendekezo ya umiliki wa raslimali zinazomilikiwa kwa jina la Mtandao

e) Katika muktadha huu wa kuvunja Mtandao, hakuna uamuzi utakaopitishwa na kuagiza kugawanywa kwa raslimali za Mtandao miongoni mwa wanachama au wawakilishi wao

f) Kwa maamuzi hayo, mali za Mtandao zitagawiwa kwenye taasisi nyingine zenye malengo yanayoshabihiana na ya Mtandao huu.

g) Hakuna rasilimali za Mtandao zitakazogawiwa, baada ya kuvunjwa kwa Mtandao, hadi kukamilishwa kwa madeni yaliyopo na majukumu yaliyofikiwa kisheria na wafanyakazi wa Mtandao kwa wakati huo

IBARA YA NANE - KUANZA KUTUMIKA KWA KATIBA HII

a) Katiba hii itaanza kutumika mara tu baada ya kuwekwa sahihi na wanachama wote wa Mtandao na baada ya kuthibitishwa na Msajili wa Asasi zisizo za kiserikali

b) Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao atasambaza nakala za Katiba hii kwa wanachama wote mara baada ya katiba hii kuanza kutumika.

c) Mtandao utafanya Mkutano wake wa Mwaka ndani ya miezi sita toka tarehe ya kuandikishwa upya kwa Katiba hii.

IBARA YA TISA - UWAJIBIKAJI

Hakuna mwanachama atakayewajibika binafsi kwa matendo , uzembe , au kukiukwa kwa taratibu za mmoja wapo wa wanachama wengine au mtumishi wa mtandao au kwa hasara au uharibifu utakaotokea kutokana na utekelezaji wa kazi za shirika lake zinazohusiana na mtandao isipokuwa kama itathibitika kuwa matendo,au uzembe huo unatokana na utashi au uzembe wa mwanachama huyo.

IBARA YA KUMI - KUTHIBITISHA KATIBA

Katiba hii imepitishwa na kuthibitishwa na wajumbe halali wa mkutano mkuu kama orodha inavyoonesha hapo chini:

Na	Jina la Mjumbe	Taasisi /shirika anayoiwakilisha	Mawasiliano rasmi	Saini ya mjumbe
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				
9				
10				
11				
12				
13				
14				
15				
16				
17				
18				
19				
20				